# DARASA LA NANE MUHULA WA TATU - 2014

# KISWAHILI: LUGHA

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

I) JINA LAKO II) JINA LA SHULE YAKO III) NAMBARI YA MTIHANI

**Soma vifungu vifuatavyo kisha ujibu maswali kwa kujaza vihasho kwenye nafasi 1 - 15.**

Mama alipozipata habari ___1___ ikabidi naye apewe huduma ___2___ kwanza. Jirani mmoja ___3___ kwenda kumpasha habari hiyo ya ___4___. Mwana ___5___ kitindamimba alikuwa amezamia ___6___ majini ___7___ mto wa Lusumu.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | alifurahi | alichupachupa | alizirai | aliomboleza |
| 2. | wa | ya | cha | la |
| 3. | alijitolea | alijitoa | alitoa | alitolewa |
| 4. | tanzia | tamasha | sherehe | karamu |
| 5. | yake | mwake | wake | mwao |
| 6. | za! | zam! | ji! | zi! |
| 7. | kwenye | kwa | ndani | kando |

Mwalimu alipandwa na hasira ___8___ ya kelele za wanafunzi. Aliamua kuwapa ___9___ kwa ___10___ masikio. Kuna wanafunzi ___11___ na ikabu ___12___ na wengine ___13___. Mwalimu alichukia sauti ile na kuamua kuwapa nyongeza. Waliondoka waki ___14___ ndani kwa ndani lakini laana zao zilikuwa kama dua ya kuku kwa ___15___.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 8. | kwa sababu | kwasababu | kwajili | kwa shauri |
| 9. | adabu | atabu | athabu | adhabu |
| 10. | kuwachuna | kuwagwara | kuwafinya | kuwakwara |
| 11. | waliorithika | walioridhi | wasioridhika | wasiorithika |
| 12. | waliyopewa | waliopewa | walipewa | walipatiwa |
| 13. | wakakuna | wakaguna | wakakimya | wakanyamaa |
| 14. | mwapisha | mwapisa | mwapiza | apa |
| 15. | mwewe | kifaranga | mkulima | jogoo |

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.***

16. Nomino joto liko katika ngeli ya ________
    A. LI - LI B. LI - YA
    C. YA - YA D. I - I
17. Kuku asiyetaga mayai huitwa ________
    A. kiweto B. tembe
    C. kidimu D. mangisi
18. Msemo ulio na maana sawa na tia tashtiti ni ________
    A. tia chanjo B. tia chumvi
    C. tia ubani D. tia kero
19. Kamilisha sentensi kwa kimilikishi kifaacho.
    Salaala! Umevunja baiskeli ya baba! Shauri ________
    A. yako B. lako
    C. yake D. chako

20. Chagua kikundi cha wadudu pekee.
A. Mchwa, nzige, panzi, mkizi
B. Shore, njiwa, konokono, mende
C. Sisimizi, chungu, nzige, kumbikumbi
D. Nge, tai, mbu, kiroboto

21. Watoto wadogo wanapenda michezo ______ watu wazima.
A. kuwaliko B. kumliko
C. kuliko D. kukuliko

22. Chagua sentensi sahihi kati ya hizi.
A. Mbona kuna kelele katika darasani?
B. Mapua yananiuma.
C. Makucha yako ni marefu.
D. Malango ya shule nyingi yamefungwa.

23. Ni neno lipi halifai kati ya haya?
A. Kusoma B. Kuimba
C. Kucheka D. Kufa

24. Andika sentensi katika usemi wa taarifa.
"Kimbieni" mwalimu alituambia.
A. Mwalimu alituambia tukimbie.
B. Mwalimu alituambia tukimbiekimbie.
C. Mwalimu alitukimbiza.
D. Mwalimu alituambia "kimbia."

25. Mtu anayependa nchi yake huitwa ______
A. mhafidhina B. mhaini
C. mzalendo D. mtoro

26. Makao ya buibui huitwa ______
A. utandu B. utando
C. tundu D. kiota

27. Chumba cha kuhifadhia maiti ni ufuo au makafani ilhali kile cha wagonjwa mahututi ni ______
A. wodi B. sadaruki
C. sandarusi D. kungawi

28. Kikembe cha nyuki huitwa ______
A. masegasega B. jana
C. kigunge D. kitumbi

29. Kanusha - Ungenialika ningehudhuria.
A. Usingelinialika nisingelihudhuria.
B. Usingalinialika nisingalihudhuria.
C. Usingenialika nisingalihudhuria.
D. Usingenialika nisingehudhuria.

30. Kamilisha methali ifuatayo.
Siku za mwizi ni ______
A. aribaine B. arobaini
C. arbaine D. aroba

***<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.</u>***

Ilikuwa mwendo wa saa tatu asubuhi wakati uwanja wa Tumaini ulipoanza kufurika taratibu. Magari ya uchukuzi, boda boda, teksi na vitututu maarufu viliwabeba na kuwatema abiria kwenye lango kuu la uwanja huo.

Hii hakika ilikuwa siku kati ya siku za kihistoria iliyokuwa imengojewa kwa raghba ya mkanja. Uwanja wa Tumaini ulikuwa kushoto mwa mji wa Pumziko <u>mkabala</u> wa barabara kuu ya Mwangaza. Uwanja huu ulikuwa maarufu sana kwa mikutano mbalimbali. Ulionekana kujaa kaumu ya watu hadi wengine kukwea miti ili kushibisha macho yao.

Jua lilitabasamu kwa uangavu na kupenyeza mionzi yake katikati ya miti ili kuleta sura ya upendo. Safu ya milima nayo ilijinega pembeni mwa mji huku vilele vyake vikikaribia kubusu mawingu ya amani. Jamii hizi zilikuwa zimeamua kubadili msimamo wao wa uhasama na uadui ambao mara kwa mara ulisababishwa na wizi wa mifugo, kutoaminiana kisiasa na mizozo ya mipaka ya mashamba. Kiini cha migogoro hii kilikuwa ni kama utandu wa saratani; ukabila na ubinafsi. Hakika jambo hili lilionekana kurudisha nyuma maendeleo na kuzua chuki kila mara.

"Naam, karibuni nyote," alianza Mzee Hekima ambaye alichukua jukumu la upatanishi. Yeye alitoka katika kijiji jirani cha Wapendanao. "Leo ni siku muhimu sana kwetu. Jambo la kwanza kuzingatia ni kuwasihi muishi kwa amani kama ndugu na kujenga umoja baina yenu. Ni jambo la kuhuzunisha kuona idadi kubwa ya mauko ikisababishwa na uhasama usio na msingi wowote. Mbona umchukie mwenzio kwa sababu ya rangi au eneo analoishi? Lazima tuwajali wenzetu pasi na kutazama masuala duni kama vile ukabila na ubinafsi.

Ndugu ni kufaana sio kufanana. Tumepoteza mali mengi na muda mwingi kwa kujengeana uadui. Fikirieni jinsi watoto wanavyodhulumiwa na kuathiriwa pakubwa. Hawana be wala te ilhali wao ndio viongozi wa kesho. Hii ni taswira mbaya ambayo haitasahaulika kamwe. Tafadhali tukomeshe maovu haya na tuishi kwa amani," alitamatisha Mzee Hekima.

Hakika mawaidha ya Mzee Hekima yalifungua <u>ukurasa mpya</u> wa amani. Hadhira ilisalimisha silaha

kama sime, bunduki, teo na panga walizokuwa wamejihami kwazo. Waliohudhuria waligawiwa vyakula vilivyokuwa vimeletwa na mashirika ya ufadhili. Maneno ya maridhiano yalionekana kugusa nyoyo zao. Furaha ilitanda na nyimbo za furaha, shangwe na vigelegele kushamiri hewani. Baada ya mkutano, kila mmoja alibaki na jukumu la kulinda mkataba wa amani na maridhiano. Maisha yalichukua mkondo mpya wa upendo, umoja na amani. Hizi ndizo zilizokuwa silaha za wananchi hawa na kukubali uamuzi wote wa kidemokrasia.

31. Ni nani aliyealikwa kama mpatanishi mkuu?
A. Mzee Mwangaza
B. Mzee Tumaini
C. Mzee Saratani
D. Mzee Hekima

32. Ni vyombo vipi havikutumiwa kubeba abiria?
A. Baiskeli, vitututu
B. Teksi, magari
C. Tuktuk, treni
D. Vitututu, bodaboda

33. Chanzo cha uhasama baina ya wenyeji hawa kilikuwa________
A. tofauti za kisiasa
B. ukabila na ubinafsi
C. ugonjwa wa saratani
D. mipaka na mashamba

34. Walioathiriwa sana na uhasama huu walikuwa ni akina nani?
A. Viongozi B. Mzee Hekima
C. Watoto D. Maskini

35. Maana ya neno mkabala jinsi lilivyotumika kwenye makala ni________
A. mbele ya B. sako kwa bako
C. nyuma ya D. kando ya

36. Ni zana ipi haikutajwa kwenye taarifa?
A. Kombeo B. Upanga
C. Sime D. Bunduki

37. Matumizi ya majina kama vile hekima, tumaini, mwangaza kama yalivyotumiwa katika taarifa huitwa________
A. tashbihi B. takriri C. majazi D. jazanda

38. Ni mambo yapi ambayo hayaonyeshi ufanisi wa mapatanisho haya?
A. Furaha na shangwe
B. Vigelegele na nyimbo
C. Kusalimisha silaha
D. Utandu wa saratani na kubeba silaha

39. Nini maana ya "yalifungua ukurasa mpya" wa amani?
A. Ukursa wa madaftari ulifunguliwa upya
B. Maisha yalianza upya
C. Uhasama na ukabila ulianza upya
D. Hadhira ilijihami

40. Kichwa mwafaka cha habari hii ni________
A. Uhasama kabambe
B. Vyakula tolatola
C. Gusa moyo
D. Amani na maridhiano

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.</u>***

Tangu nipevuke na kutofautisha baya na zuri kuna jambo ambalo limenitia kizungumkuti. Jambo lenyewe si geni machoni mwetu na pia tumelisikia likitajwa. Mwafrika ameshindwa kuuthibiti utamaduni wake. Amekuwa ng'ombe wa shemere anayejitolea mhanga kutumiwa kwa kila njia na jiha. Ametekwa na utamaduni wa kigeni. Kwa muda mrefu amemsujudia mtu mweupe kiasi cha kumwabudu. Mila zetu ziko wapi? Haya yote tumeyazibia masikio tusiyasikie na kuyafumbia macho tusiyaone. Mwacha mila chambilecho wazee wa zama ni mtumwa. Nasi bila shaka tumekuwa watumwa wa wakimwa.

Ukichambua kwa undani utapata kuona kuwa Mwafrika ameiga mambo mengi sana. Tazama dini, elimu, mavazi, maadili na mambo mengine mengi. Hebu tuliangazie jambo hili la lugha. Siku hizi nimebaki kupigwa na butwaa kuona kuwa lugha zetu za mama zinafifia. Juzi nilimwuliza banati mmoja anajua lugha ngapi. Akanieleza kuwa yeye ni Mwafrika, Mkenya ila hajui lugha yake ya kiasili. Alinifichulia kuwa anakijua Kiswahili kwa asilimia ndogo sana. Yeye mwenyewe alikiri kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu na wakati huo huo akajikanganya kwa kusema lugha hii huzungumzwa na watu ambao hawajaelimika. Alikisifu Kiingereza na Kijerumani na akanieleza jinsi ambavyo amebobea na kutopea katika lugha hizi.

Ndege mwigo hana mazoea na ukimwiga tembo kunya utapasuka mwaranda. Ni vizuri kuzithamini lugha zetu. Lugha ya Kiswahili ilipewa hadhi zake pindi mataifa ya Afrika Mashariki yalipojinyakulia uhuru..

Ni lugha ambayo ilipewa kipaumbele hata ikawa inatumika katika vikao vya bunge na sherehe maalum za kitaifa. Hata hivyo ukoloni mamboleo umekita mizizi na kuwa kizingiti kikubwa kwa maendeleo ya Kiswahili. Kiswahili kina umuhimu mkubwa katika jamii. Kwanza ni lugha yetu ya Kiafrika. Pili, lugha hii inazungumzwa kote Afrika Mashariki hivyo basi inaunganisha jamii zetu. Tatu, Kiswahili ni chombo cha kukuza ushirikiano na utangamano.

Serikali za mataifa yote ya Afrika Mashariki yaani Kenya, Uganda na Tanzania zina jukumu kubwa la kukiendeleza Kiswahili. Waswahili husema masikio hayapiti kichwa lakini hapa petu msemo huu umedhihirika dhahiri shahiri. Sisemi kuwa lugha ya Kiingereza isizungumzwe. La hasha! Lakini viongozi wa serikali zetu wakitengee Kiswahili nafasi yake ambayo kinapaswa kumiliki. Wakenya tujivunie Kiswahili. Ikiwa kuna Wamarekani ambao wanafika hapa petu kujifunza Kiswahili, na sisi je? Tayari idhaa ya BBC ni ngangari kwa miaka mingi. Sauti ya Amerika pia haijaachwa nyuma. Kuna idhaa nyingine Ujerumani na hata pia nchini China zinazotangaza kwa Kiswahili. Je, Mwafrika haoni hayo? Heko kwa marehemu Sheikh Shaaban Robert. Hongera mtafiti <u>Sheikh</u> Ahmed Nabhany. Sifa teletele zikwendee mwandishi mwenye utashi wa kuandika Ken Walibora na mwisho mshairi aso mtashi mwalimu Hassan Mbenga. Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na karama awaweke chini ya kivuli cha amani na itifaki.

---

41. Kulingana na msimulizi wa makala haya, ili mtu aweze kutofautisha baya na zuri inabidi _____
    A. aweze kuwa mtaalamu
    B. awe amekaa kutofautisha yote
    C. awe amekomaa kiasi cha kuyatofautisha
    D. awe anajua lugha zote
42. Kushindwa kwa Mwafrika kuthibiti utamaduni wake ni jambo ambalo _______
    A. limesikika likitajwa kwa nadra sana
    B. si geni, limekuwa likitajwa mara nyingi
    C. linahitaji mtu apevuke na kuelimika
    D. limemrudisha Mwafrika nyuma na kumlimbikizia umaskini
43. Watu weupe katika taarifa wamepewa jina gani?
    A. Ng'ombe wa shemere
    B. Miungu
    C. Wakimwa
    D. Watumwa
44. Kulingana na taarifa, ni methali gani isiyostahili kupigiwa Mwafrika?
    A. Vishindo vya mashua havishtui bahari
    B. Ukimwiga ndovu kunya utapasuka mwaranda
    C. Mwacha mila ni mtumwa
    D. Ndege mwigo hana mazoea
45. Mkanganyo wa fikira duni katika ufahamu huu ni _______
    A. watu kukihusudu sana Kiingereza
    B. watu kutojua lugha zao asilia
    C. watu kuwa na ari ya kujifunza lugha za kigeni
    D. watu kukidunisha Kiswahili na vilevile kukiona kigumu
46. Kulingana na ufahamu, ni wapi hasa lugha ya Kiswahili ilipewa kipaumbele?
    A. Kwenye mijadala mbali mbali bungeni
    B. Kwenye sherehe za kitaifa kama Jamhuri
    C. Wakati wa kuadhimisha sikukuu ya Madaraka
    D. Kwenye afisi ya katibu wa wizara
47. Katika kanda yetu ya Afrika Mashariki, masikio yamepita kichwa maana yake ni _________
    A. watu wameanza kuumbwa masikio yakiwa juu ya vichwa
    B. watu wameyang'oa masikio na kuyapachika vichwani pao
    C. watu wameiga tabia na nyendo za watu weupe
    D. Waafrika wamekidunisha Kiswahili na kukipa kipaumbele Kiingereza
48. Ni mataifa mangapi ambayo yametajwa katika taarifa hii?
    A. 5 B. 3
    C. 6 D. 7
49. Neno Sheikh au Shekhe limepigiwa mstari. Maana yake ni _______
    A. mtu anayekijua Kiswahili sana
    B. mtu Mwafrika halisi mwenye kuuthamini utamaduni
    C. mzee anayeheshimiwa kwa busara na mashauri anayotoa
    D. mtu mwenye elimu ya dini ya Kiislamu na aghalabu huifundisha kwa watu wengine
50. Kati ya wale watu ambao msimulizi amewavulia kofia mwishoni mwa ufahamu, ni yupi malenga?
    A.. Mwalimu Hassan Mbenga
    B. Sheikh Ahmed Nabhany
    C. Sheikh Shaaban Robert